# **HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA JAJI MKUU WA TANZANIA WAKATI WA UFUNGUZI WA KONGAMANO LA WADAU KUJADILI MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA KATIKA MFUMO WA UTOAJI HAKI NCHINI**

**KATIKA UKUMBI WA HAZINA DODOMA**

**TAREHE 17/06/2020**

**Mhe. Jaji Kiongozi,**

**Wahe. Majaji Wafawidhi,**

**Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu mliopo,**

**Mhe. Mkuu wa Chuo Lushoto**

**Wahe. Makamishna Tume ya Utumishi wa Mahakama,**

**Mkurugenzi wa TAKUKURU Brigedia General John Mbung'o,**

**Mhe. Mtendaji Mkuu wa Mahakama,**

**Mhe. Msajili Mkuu,**

**Kaimu Mkuu wa Law School, Bwana Zakayo Lukumayi**

**Wahe. Wasajili,**

**Wahe. Wakuu wa Wilaya mliopo,**

**Watendaji wa Mahakama,**

**Mwakilishi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**

**Mwakilishi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria,**

**Mwakilishi kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**Wawakilishi wa Taasisi mbali mbali za umma mliopo,**

**Mabibi na Bwana.**

Awali ya yote nichukue fursa hii adhimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia siha na afya njema kukusanyika mahali hapa leo katika Kongamano hili muhimu kuhusu Mapambano dhidi ya Rushwa katika Mfumo wa Utoaji Haki.

Nichukue nafasi hii pia kuungana na Mheshimiwa Jaji Kiongozi kuwashukuru nyote mlioitikia mwaliko wa kuja kuungana nasi katika Kongamano hili la aina yake ambalo linatoa fursa ya kujadili hali ya rushwa katika vyombo vya

utoaji haki, changamoto zilizopo, lakini pia mikakati iliyopo ya kukabiliana na rushwa katika vyombo vyetu vya utoaji haki nchini.

Kipekee niwapongeze wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanya maandalizi haya ambayo natambua kuwa yamefanyika kwa muda mfupi sana kutokana na changamoto zilizoletwa na janga la ugonjwa wa mapafu (COVID-19). Kwa kiasi kikubwa janga la COVID-19 libadili maisha yetu ya kila siku, ikiwemo mipango ya kuandaa kongamano kama hili la leo.

Hata hivyo, nafarijika kuona kuwa muda mfupi baada ya hali ya janga kutulia, maandalizi yamefanyika na leo hii tuko pamoja. Hongereni sana.

Pia napenda sana kuwashukuru BSAAT ( Building Sustainable Anti- Corruption Action in Tanzania) hawa katika mpango wa miaka mitano wa kupunguza rishwa wamefanya kazi kubwa sana, kupitia mpango wao wameweza kuongeza uadilifu na utawala bora , pia mpango

huu umekwenda sambamba na mpango kabambe wa kupambana na rushwa wa taifa ( NACSAP III)

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana TAKUKURU kwa kufanya utafiti katika mahakama na kutuonyesha maeneo yenye viashiria vya rushwa, hii imetusaidia sana katika kabiliana na rushwa sisi wenyewe.

**Vita dhidi ya Rushwa hufanikiwa kwa kushirikiana**

Kongamano la leo ni kielelezo cha umuhimu wa taasisi za utoaji haki kushirikiana katika vita dhidi ya rushwa, na umuhimu wa Mhimili wa Mahakama kushirikiana na taasisi zingine.

Umuhimu wa kushirikiana katika vita dhidi ya rushwa ulitambuliwa mwaka 2003 wakati Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilitunga Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Rushwa (the United Nations Convention Against Corruption) ambao ulianza kufanya kazi tarehe 14 Disemba 2005.

Mkataba huu uligusia ukweli kuwa Mhimili wa Mahakama hautafanikiwa katika vita dhidi ya Rushwa endapo itasimamia vita hivyo peke yake bila kushirikiana na wadau na taasisi zingine.

Ingawa tunasema tuhuma nyingi dhidi ya rushwa dhidi yetu ni hisia (perception) lakini hatuwezi kuzidharau hizo hisia, kwa sababu rushwa hujificha nan wananchi na mwananchi wa kawaida anapopata huduma ndio anayokutana nayo.

**ROBO KARNE YA TUME YA RAIS KUHUSU RUSHWA *(REPORT OF THE PRESIDENTIAL COMMISSION ON CORRUPTION—TUME YA WARIOBA)***

Kongamano la wadau katika mapambano dhidi ya rushwa ni wakati mzuri sana wa kubadilishana uzoefu, kujitathmini na kujifunza kutoka kwa wengine.

Tunapokusanyika hapa leo katika kongamano hili muhimu kuhusu changamoto ya rushwa katika mfumo wa

utoaji haki, ni vyema tukatafakari kuwa tunakaribia robo karne tangu TUME YA RAIS KUHUSU RUSHWA (REPORT OF THE PRESIDENTIAL COMMISSION ON CORRUPTION— TUME YA WARIOBA).

Tarehe 7 Disemba 1996, Mhe. Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa alikabidhiwa Ripoti ya Tume ya Warioba. Mwaka ujao, tarehe 7 Disemba 2021, Ripoti hiyo itakuwa imetimiza miaka 25 (robo karne) tangu ilipowasilishwa. Tunapojadiliana leo changamoto ya rushwa katika mfumo wa utoaji haki, pengine itakuwa ni vyema tujitayarishe hapo mwakani kufanya TATHMINI KUBWA YA HALI YA RUSHWA na kujipima ni kwa namna ghani kila taasisi katika mfumo wetu wa utoaji haki, umeshughulikia mianya ya rushwa, viashiria vya rushwa iliyobainishwa na Tume ya Warioba miaka 25 iliyopita.

Katika kitabu cha Mhe. Benjamini William Mkapa, ( My life, My Purpose) ukurasa wa 203 akiinukuu Tume ya

Warioba ameeleza kuwa Mahakimu 43 walifukuzwa kazi na madalali watano leseni zao zilisitishwa.

Aidha mnamo tarehe 16/12/1996 Mhe Rais Mstaafu Benjamini William Mkapa akifungua semina ya Majaji na Mahakimu juu ya Mapambano dhidi ya Rushwa alitambua mchango mkubwa wa Mhimili wa Mahakama katika mafanikio ya maboresho ya kisiasa na kiuchumi. Lakini mhimili wa mahakama hauwezi kusaidia katika uendelevu wa maboresho endapo itatajwa vibaya katika ripoti ya Rushwa.

**Ndugu washiriki,**

Mjadala wa rushwa ni mpana sana na ninatambua kuwa hauwezi kukamilika kwa siku moja. Hata hivyo nimefarijika kuona kuwa kutakuwa na wawezeshaji ambao watatoa mada kuonyesha ni nini Mahakama ya Tanzania imefanya na inaendelea kufanya katika kukabiliana na rushwa kupitia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano

(2015/16-2019/20) ambao unaelekea ukingoni na kwa sasa maandalizi ya Mpango Mkakati wa Miaka mingine mitano yako mbioni.

Hatahivyo kwakuwa hatuwezi kutenganisha majukumu yetu ya kila siku na vita dhidi ya Rushwa. Ni matumani Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, itatumia fursa ya siku ya leo, kutuelewesha namna inavyotumia Mpango Mkakati wake wa miaka Mitano kama nyenzo muhimu katika kupambana na rushwa KIMFUMO, KIMKAKATI na KIMUUNDO. Kwa mfano, MPANGO MKAKATI WA MAHAKAMA NA PROGRAMU YAKE YA MABORESHO imesimama kwa kutumia nguzo tatu. Hapa ninasema kuwa, huwezi kutenganisha vita dhidi ya rushwa na wajibu wetu wa utoaji huduma za kila siku:

**I.-Utawala bora, uwajibikaji na usimamizi wa rasilmali.** Rushwa hushamiri katika taasisi za utoaji haki ambazo hazina utawala bora. Rushwa hushamiri

pale ambapo hakuna uwajibikaji na pale ambapo hakuna usimamizi bora wa rasilmali.

**II.-Upatikanaji na utoaji wa haki kwa wakati**: Ni silaha muhimu dhidi ya rushwa. Rushwa hushamiri katika taasisi ambayo inachelewesha haki.

**III. Imani ya wananchi** ni silaha muhimu sana katika vita dhidi ya rushwa katika taasisi za utoaji haki. Taasisi zinazohusika na utoaji haki zikishirikiana, nafasi ya rushwa kushamiri hutoweka. Mwananchi ambaye ndiye mdau mkuu anapaswa kuwa na imani na mfumo wa utoaji haki ambao ndio kimbilio la wale wenye kudai haki zao. Iwapo wananchi watakosa imani na mfumo wa utoaji haki upo uwezekano mkubwa wa wananchi kujichukulia sheria mkononi na hivo kuhatarisha amani na utulivu ambao ndio tunu ya Taifa letu.

**Hali ya Rushwa na Mtizamo wa Wananchi (Perception)**

Hali ya Rushwa katika Taasisi zetu katika utoaji haki hupimwa na wananchi zaidi kwa mitizamo/hisia (perception) kuliko uhalisia kwa sababu, rushwa hujificha na hujigeuza **(mutate)** ili kuepuka kuonekana, kwa hiyo bado tutaendelea kutegemea wananchi wa kawaida wanatuonaje katika mapambano dhidi ya rushwa? Mahakama imetumia mbinu nyingi ili kuibua na kupima hiyo mitizamo na hisia waliyonayo wananchi:

- Mabango
- Kujitathmini kupitia utafiti uliofanywa na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya REPOA 2015, 2019 [*Ilipima—(i)-uridhishwaji na huduma za mahakama; (ii)-upatikanaji wa taarifa muhimu za mashauri; (iii)-Je huduma zinazotolewa na Mahakama zinamlenga mtumiaji wa huduma za Mahakama?*]

**Tuwasikilize wanananchi, na tuwape nafasi ya kutukosoa**

Siku hizi kumezuka tabia katika utumishi wa umma wa kutowajibu wananchi wanaoandika barua za malalamiko. Tusiwazuie wananchi kulalamika kwa sababu malalamiko yao yanaweza:

(1) kutufumbua macho kuhusu tatizo la rushwa lililojificha ndani ya taasisi zetu;

(2) Lalamiko linaweza kutupa jicho la ziada la kuangalia sharia na taratibu zetu kwa undani na kugundua mapungufu yanayohitaji marekebisho;

(3) Inaweza kutupa tahadhari kuwa wananchi hawaelewi sheria na taratibu na wanahitaji kuelimishwa Zaidi kuhusu namna ya kupata haki.

Hivyo basi, wananchi ndio kioo chetu cha kujipima, ni jukumu letu kuwasikiliza na kujisahihisha.

Niseme tu kuwa maboresho yanayofanywa na taasisi yoyote iliyo katika mfumo wa utoaji haki Tanzania

hayatokuwa na maana yoyote, iwapo suala la rushwa katika vyombo vya utoaji haki litafumbiwa macho na pale ambapo hatuwasikilizi wananchi wanaokuja kupata huduma kutoka kwetu.

Aidha, mapambano dhidi ya rushwa kwa chombo kimoja cha utoaji haki hayatokuwa na maana iwapo vyombo vingine vitaendelea kufumbia macho jinamizi la rushwa.

Nimefarijika kuona kuwa katika ratiba kuna fursa ya jopo la wadau kutoka vyombo mbali mbali kutoa maoni na michango yao kuhusu mchango wa vyombo vingine vya utoaji haki ukiachia mahakama katika kupambana na rushwa. Hii inatokana na ukweli kuwa utoaji haki ni mnyororo mrefu unaohusisha wadau mbali mbali na vyombo mbali mbali pia.

**Ndugu washiriki,**

Kila mmoja wetu anayo nafasi na wajibu wa kushiriki katika vita dhidi ya rushwa. Utashi wa kisiasa na dhamira

anaouonyesha Mhe. Dr. John Pombe Joseph Magufuli haitoshi bila ya kila Taasisi, kila mwananchi kukubali kwa vitendo kuwa sehemu ya vita dhidi ya rushwa.

Katika majadiliano yetu leo, pamoja kujadili sheria na Taasisi, tusisahau kuwa ufanisi wa Sheria na Taasisi katika kupambana na rushwa kwa kiasi kikubwa inategemea kwa kiasi gani jamii na wananchi wa kawaida wanavyokubali kushiriki katika vita dhidi ya rushwa.

Yapo baadhi ya maswali ambayo ni muhimu kumuuliza mwananchi wa kawaida, ili kumfahamu kama kweli anachukia rushwa kwa vitendo na kwa moyo wake wote:

1.-Je anamchukulia kiongozi/mtumishi anayependa rushwa kama shujaa?

2.-Wananchi/watumishi wapo tayari kutoa taarifa ya vitendo vya rushwa na wanakubali kuwa mashahidi katika mashauri ya rushwa?

3.-Je ndugu, jamaa, familia zetu zinatushawishi kushiriki katika rushwa?

Niwasihi mtumie fursa hii kujadili kwa uwazi na kina changamoto tulizonazo bila kutupiana lawama kwani sisi sote tunajenga nyumba moja na hivo hakuna sababu ya kugombea fito kwa maana ya kunyosheana vidole.

**Ndugu washiriki,**

Napenda kutoa msisitizo kwamba, Mahakama ya Tanzania imekubali kuwa juhudi la kujisafisha mbele ya macho ya wananchi ni lazima zianzie ndani ya taasisi husika. Ndio maana ukifika maeneo ya Mahakama utakaribishwa na MABANGO yanayotoa namba za simu za kutoa taarifa kuhusu vitendo vya rushwa.

Malengo ya maboresho ya Mahakama ya Tanzania hayatafanikiwa iwapo suala la maadili hayatapewa mkazo.

Uhuru wa Mahakama unaimarika pale kunapokuwa na uwajibikaji kwenye maadili ikiwemo kupinga kwa hali zote vitendo vya rushwa.

Mahakama ya Tanzania kupitia hatua na juhudi mbali mbali, imeonyesha nia na dhamira ya dhati kabisa katika kupiga vita vitendo vya kuomba Rushwa.

Jitihada dhidi ya vitendo hivi zitafanikiwa tu endapo wananchi watawasilisha taarifa za **KWELI** za **MATUKIO** ya ukiukwaji wa Maadili mbele ya Kamati za Maadili, na Kamati hizi zifanye kazi kwa mujibu wa miongozo na taratibu zilizowekwa. Rushwa na utovu wa Maadili haina nafasi katika Mahakama inayofuata misingi ya maboresho.

Niseme pia suala la utoaji haki ni suala mtambuka. Ibara 107A inasema " mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakuw ani mahakama, neno " ya mwisho" inamaanisha sio mamlaka pekee inayotoa haki ziko taasisi nyingi za umma zinazotakiwa kutoa haki mfano kupeleleza, kuendesha mashtaka, kutoa leseni n.k. Hata watumishi wa umma yapo maswala yanayogusa Haki ambayo mwananchi hana nafasi ya kuja mahakamani.

**Ndugu washiriki,**

Ni mategemeo yangu mimi binafsi na Mahakama ya Tanzania kuwa wadau wa mkutano huu mtatumia fursa hii kutoa maoni yenu na ikibidi kuja na maazimio yenye lengo la kupunguza kama sio kuondokana na vitendo vya rushwa katika mfumo wa utoaji haki. Naamini kuwa Kongamano hili halitakuwa la mwisho bali mwanzo wa makongamano ya namna hii siku za usoni.

**Ndugu washiriki,**

Niwahakikishie kuwa Kongamano hili la kujadili mapambano dhidi ya rushwa tutajitahidi lifanyike mara kwa mara ikibidi kila mwaka na kama itawezekana liwe zaidi ya siku moja na hivyo basi maoni yenu kuhusu namna bora ya kuboresha Kongamano hili siku za usoni ni muhimu sana.

**Ndugu washiriki,**

Kwa maneno haya machache naomba nitamke kuwa Kongamano hili la wadau kujadili mapambano ya rushwa katika mfumo wa utoaji haki limefunguliwa rasmi.

***Ahsanteni kwa kunisikiliza!***